# *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*

Mnajua, wahubiri daima huchosha kwa mazungumzo marefu, nami ndivyo nilivyo. Kwa hiyo mimi . . . Nadhani tuna dakika chache tu, kama dakika kumi ama kumi na tano, kitu kama hicho? Nami ningependa tu kusema ya kwamba bila shaka nimefurahia kukaa huku pamoja na nyinyi—nyinyi marafiki. Na asubuhi ya leo, nikiingia na kukutana na Dada, hapa, ambaye nilikuwa nimemwona katika ono kule, hivi majuzi usiku, nikaja kugundua kwamba alikuwa . . . a—alikuwa na ugonjwa wa Hodgkin wakati mmoja mkutanoni, naye akaponywa, na mara tatu mbalimbali ambapo Roho Mtakatifu amemtaja mwanamke huyu.

2 Halafu basi, nilikutana na ndugu huyu hapa, ambaye, huko kwenye mkutano mwingine, alikuwa na kansa usoni mwake. Na jinsi Bwana amemponya, na . . . [Ndugu fulani anasema, "Jackson."—Mh.] Ndugu Jackson, mpiga kinanda. Ndipo basi nikakumbushwa, huko Lakeport, ambako tulikuwa na mkutano kule juu hivi majuzi, na kulikuwako na maskini Mjerumani, ama mtu fulani upande wa pili wa kilima, naye alikuwa na mke wake amelala kule. Naye Roho Mtakatifu alikuwa akifanya upambanuzi, na kumwambia jinsi alivyokuwa ametoa ahadi kutoa kiasi *fulani* cha pesa kwa kanisa kama Bwana angemjalia mke wake aponywe kansa, na kumwambia ya kwamba—ya kwamba haikumbidi kutoa ahadi hiyo, Mungu anamiliki kila kitu kwa vyovyote vile. Na kwa hiyo wao . . . Naye huyo mama akaponywa, angali anaishi na kuninii tu . . . Nilimwona.

3 Basi mnamo wakati huo wakapiga picha ya Malaika wa Bwana akiwa amesimama pale, na kulikuwa na . . . rangi hiyo ya upinde wa mvua. Wengi wenu ninyi watu mmeiona hiyo picha.

4 Ndipo nikaja kugundua ya kwamba ndugu yetu mwenyekiti, nilifikiri tulikuwa ndugu kamili, ndipo nikaja kugundua yeye—yeye ni Muarkie. Hivi wewe . . . ? Naam, bwana. Naam, bwana. Nao wananiambia kama ukiondoa Arkansas na Oklahoma kutoka California, hakungekuwako na California tena. Vema, hakika kumekuwa na marafiki wazuri sana kutoka Arkansas. Nami nina hakika kama nitawahi kufika Mbinguni nitaona watu wengi huko kutoka Arkansas, na Oklahoma, na ulimwengu mzima. Tuna furaha sana kuwa hapa, tukiwa na wakati huu wa ushirika.

5 Basi mtu fulani alikuwa akiniambia ya kwamba maskini mama mmoja, hapa mahali fulani, ambaye alikuwa na . . .

katika...Ninaamini ni mama huyu papa hapa, ninii...mtu huyu na mkewe, alisema ya kwamba aliitwa jana usiku, mkutanoni, kuhusu kuwa na namna fulani ya uvimbe, ama kitu fulani, mwilini mwake. Na watu mbalimbali...Niliwazia labda katika wakati huu kwamba ningejaribu kuelezea kidogo.

6 Sasa, wewe angalia saa yako, na usione haya kushika koti langu wakati ukikaribia tu, maana ni—ninapoanza kuzungumza. Sitamwambia *yeye*, tayari anavuta. Mnaona? [Dada mmoja anasema, "Vema, tunaufurahia."—Mh.] Na kwa hiyo, najua, lakini sisi—sisi...chumba hiki hapa, labda watakihitaji. Hicho si kilikuwa ni kiamshakinywa cha kupendeza? Si...Kweli mngekithamini hicho! Hicho kilikuwa ni kiamshakinywa halisi cha Arkansas, hiyo ni kweli, hemu na mayai, na kadhalika.

Na kwa hiyo, mikutano hapa, tulijisikia ya kwamba Bwana atatuongoza hapa juu, na kuwa na wakati huu wa ushirika, na kweli umekuwa mzuri.

7 Sasa, maono ni kitu cha kipekee. Tulikuwa tumeketi hapa tukizungumza kuhusu huko nyuma kwenye ile mikutano ya mwanzoni, jinsi ambavyo watu waliendesha magari, baadhi yao wangekuja maili elfu tatu, teksi, kufika mkutanoni. Sasa, kumbukeni, Yeye ni Mungu tu sasa kadiri alivyokuwa wakati huo. Mnaona? Nayo hu—hu—huduma tangu hapo hadi wakati huu imeboreka kwa asilimia mia moja, mnaona, mnaona, huduma. Lakini ro—roho ya uamsho inawaacha watu, mnaona, inatoweka. Haionekani kama watu wana shauku waliyokuwa nayo.

8 Sasa, hivi ndivyo maono yanavyofanya. Sasa, ninii... dada yetu hapa, jambo la ajabu, nilipogeuka hivi majuzi usiku, nikimtazama Ndugu, naye alikuwa akinisimulia hadithi ya kuketi pale chini kuutazama uso wake, mnaona, na—na kumwona mwanamke huyu, ndipo nikaangalia nyuma tena, nami nikaona ilikuwa ikitoka upande *huu*, nikaangalia, na huyo hapo yule mwanamke, na hapa sikuwa na fununu hilo lingekuwaje, mwajua, wala sikujua, kwamba ni mkewe, ndipo nikaona ono likifunguka basi, ilikuwa ni nyumbani mwao, nami nilijua ilibidi iwe ni mkewe basi. Na hiyo ni mara tatu ambapo amefanya hivyo.

9 Sasa, jambo hilo ni kwamba, ni imani yake katika karama hiyo. Mnaona? Yeye hatambui, bali yeye ndiye anayefanya jambo hilo. Analifanya mwenyewe. Sasa, kama tukiwazia tu kwa dakika moja, labda mimi...ili mpate kufahamu vizuri zaidi jinsi ilivyo katika dakika hizi chache, hebu na tumchukue Bwana wetu, kwa sababu, hata hivyo, kila kitu ni Chake. Mnaona? Ni Yeye, wala sio sisi, isingeweza kuwa mmoja wetu sisi ndugu wahudumu wala mtu yeyote. Ni...

10 Hatudai kuihubiri Injili kwa akili zetu wenyewe, tunaihubiri kwa nguvu za Mungu. Ninyi wahudumu mnafanya hivyo. Na

hizo ni nguvu za Mungu zinazokuja juu yenu na kuwatia mafuta. Na hata katika ninii yako . . . huduma yako unasema mambo, na wakati mwingine wewe: "Kwa nini nikabadilisha somo langu?" Nanyi mnajua jinsi ilivyo. Mnaona? Huyo ni Mungu akifanya jambo hilo, mnaona. Na Yeye—na Yeye . . . Huenda ukafikiri ya kwamba kusanyiko lote lililikosa, na labda mtu mmoja mdogo anayeketi pale, Mungu alikuwa akiuelekeza ujumbe huo wote moja kwa moja kwa mtu huyo mmoja.

11 Na wakati mwingine umeona ulishuka moja kwa moja mstarini ukihubiri, ukisema "*Hili* ndilo. *Hili* ndilo." Halafu basi wakati mwingine, unageuka na kusema kitu fulani kinachoonekana kupinga hilo. Unawazia, "Kwani mimi ni mnafiki?" Mnaona? Lakini, unaona, ni Mungu akitenda kazi ndani yako, kama nilivyosema juu ya Yona hivi majuzi usiku. Mnaona, yeye hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana, ilikuwa ni Mungu akitenda kazi ndani yake. Yeye alimtuma kwa njia moja, lakini alikuwa . . . akamtuma . . . akamwambia aende huko, lakini akamgeuza. Mnaona?

12 Hivyo ndivyo, wakati mwingine nimesema mambo, nami ninageuka na kuwazia, "Kwani nina shida gani?" Ninakuja kugundua, ni Roho Mtakatifu. Na wakati mtu, akihubiri kwa uvuvio, hana budi kujitolea kabisa kwa Roho, ndiyo njia pekee tutakayowahi, au, ninayoweza kufanya hivyo, maana sina nguvu za kiakili za ku—kuweka mahubiri ama chochote kile pamoja.

13 Nanyi ndugu wahudumu, wakati tukiwa pamoja, ni—nimesema hili kutoka jukwaani, ninataka kulisema tena, nimeuweka mkutano huu kitoto kwa namna fulani, mwajua, kwa namna fulani . . . kusudi watu, kuna wengi wao hapa . . . Ninatambua nchi hii, ya kwamba hii ni nchi kuu ya Kikatoliki, haina budi kuwa hapa, mnaona, nao hao watu wanaoingia tu, wananinii tu, hawalipati kama ukiingilia kitu kigumu.

14 Sasa, hebu na tumchukue Bwana wetu kama Mfano wetu kwa sababu Yeye alisema alikuwa Mfano wetu. Sasa, Uhai Wake uko ndani yetu. Sasa, tungewazia hivi, ili kwamba tupate tu wazo dogo la, sio somo la kuhubiria, lakini Yesu alisema wakati mmoja, akinena kuhusu ndoa na talaka, Yeye alisema, *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*.

15 Sasa, itatubidi kurudi kwenye mwanzo ili kupata kila kitu, kwa sababu kila kitu kilikuwa na mwanzo, tunachoona sasa. Vitu vya Milele ndivyo havikuwa na mwanzo, maana *Milele* kamwe haikuanza, haina mwisho. Basi ni vitu vilivyo na mwanzo ndivyo vilivyo na mwisho, kila kitu. Sasa, Mwanzo ni mlango wa mbegu, kwa hiyo itatubidi kurudi kwenye Mwanzo.

16 Nasi tukichunguza kupitia vitabu vingi vya historia ya Kanisa, *Babeli Mbili* (cha Hislop), labda mumekisoma, na Kitabu Cha *Wafia Imani* cha Foxe, na—na *Baraza Lililotangulia Nikea*, *Wazee wa Nikea,* na ka—kadhalika, unarudi na kuona ya

kwamba kila roho nchini, na kila dhehebu, na kila kitu, kama ukirudi nyuma, kilianza katika Mwanzo. Unakaribia wakati wa kuchanua, wakati wa kuchanua. Unawaona wakitokea kama Kaini na Habili, na hebu waangalieni hao wavulana wawili wakishuka moja kwa moja kuwa Yuda na Yesu, na kuendelea moja kwa moja, mnaona. Inakuja moja kwa moja kufikia siku hizi za mwisho, ambapo mpinga-Kristo na Roho wa Kristo, wanafanana sana, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Sasa, tunafundishwa hilo, nasi tunajua hilo ni kweli.

17 Sasa, tumchukue Bwana wetu, wakati alipokuwa hapa hakudai kufanya miujiza, alisema ilikuwa ni Baba, Mungu, aliyekaa ndani Yake, Naye alikuwa. . . Alimdhihirisha Mungu kupitia kwake Mwenyewe. Mungu, vinginevyo, alijijengea Mwenyewe mwili ambao aliishi ndani yake Mwenyewe. Mungu alishuka, akadhihirishwa katika mwili ndani ya Kristo, wala haikuwa ni Yesu, ule mwili, Mwana wa Mungu, ilikuwa ni Mungu wa Utukufu katika Mwana wa Mungu, akionyesha utukufu wa Mungu, mnaona, kupitia Yeye Mwenyewe. Mungu wa Utukufu akidhihirisha utukufu wa Mungu. Na ndani Yake, Mungu alikaa ndani Yake, Naye alimwakisi Mungu.

18 Sasa, hivyo ndivyo kila mmoja wetu wahudumu anavyofanya, tunamwakisi Mungu, kama vile Mungu alivyo ndani yetu. Halafu basi, hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu anaweza kusonga, ni. . . na watu wanaweza kumwona Mungu, ni kupitia sisi, watumishi Wake. Hivyo ndivyo. . . Watu hawatasoma Biblia, bali watakusoma wewe. Unaona? Na kwa hiyo unamwakisi Kristo, mienendo yako, mazungumzo yako, matendo yako yote yanamwakisi Kristo.

19 Huenda usifikiri ni. . . watu wanakuangalia, bali wanaangalia kila hatua unayopiga, wewe ni Biblia kwa watu wengi. Kwa hiyo, hatuna budi kuangalia kile tunachofanya, mikataba yetu ya biashara, na kila kitu tunachofanya katika mwenendo wetu wote. Jisalimishe tu kwa Roho, na Mungu atajiakisi Mwenyewe kupitia kwako, kama nilivyosema, kama mzabibu. Yesu alisema katika Yohana 15, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Vema, sasa kumbukeni, mzabibu hauzai tunda, tawi ndilo linalozaa tunda, bali hupata uhai wake kutoka kwa mzabibu.

20 Vema sasa, miezi michache iliyopita nilikuwa huko Arizona kwa rafiki yangu mpendwa, John Sharrit, naye anamiliki vijisitu vingi vya michungwa. Ndugu maskini kwelikweli, ndugu Mpentekoste, naye Bwana alimbariki, na sasa anamiliki. . . yeye. . . Vema, yeye, hivi majuzi nafikiri, alikuwa akiniambia kuhusu, alikuwa na ekari arobaini na tisa elfu za pamba na kadhalika wakati huo, ambazo ninii tu. . . kile. . . Bwana amembariki kwa njia ya kifedha. Naye anaenda huku na huku akiendesha Chevrolet kuukuu, na ki—ki—kioo cha jua kinaning'inia chini.

21 Nasi tulikuwa. . . Alikuwa akinionyesha mti uliokuwa na yapata matunda matano ama sita mbalimbali, aina mbalimbali za matunda, kwenye mti huo mmoja. Sasa, ulikuwa ni mchungwa kwanza, bali walikuwa wamepandikizia mchungwa huu limau, chenza, kangaja, na ba—na ba—balungi; na tunda lolote la jamii ya chungwa lingekulia kwenye mzabibu hu—huo, kwenye mti huu.

Nami nikasema, "Ajabu hiyo, Ndugu Sharrit. Sasa," nikasema, "sasa, mwaka ujao, mazao ya pili yatakapokuja, yote yatakuwa ni machungwa."

22 Akasema, "Loo, la, huh-uh." Kasema, "M—mzabibu. . . tawi ambalo ni tawi la balungi litazaa balungi, na limau litazaa limau."

Nikasema, "Sasa, ngoja kidogo, kwenye mchungwa?"

Kasema, "Naam, yote ni matunda jamii ya chungwa, bali litazaa kwa jinsi yake, tawi lililo ndani yake."

Ndipo nikasema, "Sasa, kama huu—kama mti fulani huu, basi, utazaa tawi lingine wenyewe, litakuwa nini?"

Akasema, "Kama lile la asili; litakuwa m—mchungwa."

Nikasema, "Nimelipata." Unaona?

23 Sasa, Kristo ndiye Tawi, uh, Yeye ni M—Mzabibu. Lakini kama tukipandikiza katika. . . Asubuhi ya leo, hapa, huenda kukawa na madhehebu mbalimbali miongoni mwetu: Assemblies, Oneness, na—na Church of God, na—na makanisa haya mengine yote mbalimbali, madhehebu. Mnaona, kama tukichukua tawi letu la kimadhehebu na kuliweka Mle ndani, litazaa tu tunda la kimadhehebu. Hapo ndipo tulipo, katika mstari wa Kikristo wa jina la Kikristo, la maisha ya Kikristo, kama tunda jamii ya chungwa, tumepandikiza Kule Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, Katoliki, aina zote mbalimbali ziko chini ya jina hilo la "Ukristo."

24 Lakini hivi mliona? Wakati huo Mti wa asili ulipotoa tawi hapo mwanzo, Mti huo ulipozaa tawi Lake la kwanza, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Nayo. . . Makanisa haya, madhehebu, yanaishi kwa Mti huu jamii ya chungwa katika jina la Ukristo, lakini kama huo Mti wa kweli ukipata kuchipusha tawi lingine, wataandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake, hiyo ni kweli, mnaona, kwa sababu utazaa tunda.

25 Na sisi kama wahudumu hatuna budi kuyaacha maisha yetu yawe, si katika madhehebu fulani, mambo hayo ni sawa kudumisha udugu na kadhalika, ninamaanisha, lakini, yana mahali pao, bali sisi wenyewe lazima tujisalimishe kabisa katika Kristo, kusudi Roho Mtakatifu aweze kutiririka kupitia kwetu, mnaona. Na hiyo huzaa tunda asili la Pentekoste, ambalo ni. . .

tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, na, mwajua, kitu hicho halisi.

26 Sasa. Ninii tu. . .Sina budi kusimama sasa, lakini hapa, wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alikuwa ndiye ule Mzabibu. Yeye alileta lile Jiwe la Kichwa, tunajua, tunatambua hilo, Yeye alikuwa wa kwanza. Sasa, hebu tumwangalie alipokuwa akizunguka-zunguka, hakuzunguka huku mavazi Yake yakiwa tofauti na watu wengine, hakuwa na matendo tofauti, Yeye, Jamaa mpole tu, kama nilivyohubiri siku moja juu ya—juu ya *Heri Iliyosahaulika*.

27 Inapatikana katika Mathayo mlango wa 11 na kifungu cha 6, ambapo Yohana Mbatizaji alikuwa ameagizia kwanza, mwajua, na kuwatambulisha kwa Masihi. A—alikuwa nabii mkuu, Yohana, kati ya nyakati hizo mbili, kati ya torati na neema. Naye alikuwa amehubiri ya kwamba nanii . . . kuna Masihi ajaye ambaye atausafisha sana uwanda Wake, na kukusanya Punje, Naye atakuwa Masihi m—mkuu ambaye ataiangamiza milki ya Kirumi.

28 Ndipo Yohana akangojea nyikani mpaka alipokuwa na hakika angejua hiyo ilikuwa ni ishara gani. Kamwe hakwenda shuleni, mnakumbuka, Yohana alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa. Alikuwa na—alikuwa na agizo kutoka kwa Mungu, isingeweza kuwa ni du—duara ya kikanisa kukizunguka kitu fulani, ilibidi iwe ni halisi. Kwa hiyo akangojea nyikani mpaka aliposikia kutoka kwa Mungu.

Ndipo Mungu akasema, "Utamjua, kwa sababu kutakuwa na ishara juu Yake. Utaiona ishara hii, na huyo atakuwa ndiye Masihi."

"Naye Yohana akashuhudia, akisema, 'Nilimwona Roho wa Mungu kama hua akishuka juu Yake.'" Naye akatangaza hadharani, "Huyu ndiye Masihi."

29 Lakini basi, kulikuwa na jambo fulani lililotukia, masikitiko, hayo ndiyo yanayotupata sisi sote. Katika uponyaji wenu na kadhalika, mtaona, inaonekana kana kwamba kitu fulani hakikufanya kazi sawasawa kabisa. Kumbukeni, huyo ni adui, naye Mungu anamruhusu akupe jaribio lake, aone utakalofanya.

30 Sasa, badala ya ninii . . . Yesu akija kama vile Yohana alivyosema angekuja . . . Naye Yohana akaona ile ishara na kujua ilikuwa ni Yeye, alimtambulisha kwa umma, "Huyo Ndiye, kwa kuwa ninaona ishara ambayo Mungu aliniambia." Lakini wakati alipopata matatizo, nalo jicho lake la tai likaingia utando, kama vile Pember alivyosema, wala hakuona vizuri sana, aliwazia, "Hapa, nilihubiri ya kwamba Masihi atawaweka watu huru, na hapa maskini Jamaa mdogo, mpole, amesukumwa *hapa* na *pale*, Masihi wa ajabu."

31 Lakini kile asingeweza kuelewa, kulikuwa na ishara juu Yake lakini hata hivyo Yeye alikuwa tofauti sana. Yeye hakuwa yule jamaa mashuhuri aliyekuwa akitoka na kurarua kila kitu, kama alivyodhania angefanya, Yeye alikuwa ni Jamaa mdogo, mnyenyekevu, mpole, aliyesukumwa kutoka *hapa* kwenda *pale*, mwajua, "Jamaa huyu wa ajabu ni nani, Jamaa huyu ni nani?"

32 Kwa hiyo akawatuma wawili wa wanafunzi wake, na kusema, "Nendeni mkamwulize, Yeye Ndiye?" Sasa, hiyo ilikuwa ndiyo sifa duni sana ambayo angaliweza kumtolea Yesu, baada ya kutangaza ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi, kisha anarudi na kusema, "Hivi huyo Ndiye?" Lakini Yesu anaelewa udhaifu wetu. Akageuka na kutoa sifa kuu sana ambazo Yeye angeweza kumpa mtu yeyote, kwa Yohana.

Mwangalie Yeye, wakati Yohana alipokuja na kusema... wakati Yohana alipowatuma wanafunzi wake, walikuja, kasema, "Wewe Ndiye, au tumtazamie mwingine?"

33 Sasa, Yesu kamwe...Mwajua, Yohana alikuwa gerezani naye Yesu alijua hilo. Kwa hiyo, Yeye—Yeye kamwe hakumpa kitabu cha jinsi ya kujiadibisha gerezani, ama—ama kitu kama hicho, au kumwambia baadhi ya desturi na kanuni za uamsho, Yeye alisema tu, "Kaeni na mngoje mpaka ibada iishe ndipo mwende mkasimulie mlichoona."

34 Kwa hiyo wakati...Wakawaona viwete wakitembea, vipofu wakiona. Nami ninaweza tu kuwazia kumwona Bwana wetu amesimama pale, wakati hao wanafunzi wakipanda kilimani, Naye akawaangalia, akageuka na kusema, "Mlitoka kwenda kuona nini? Mlitoka kwenda kuona u—unyasi unaotikiswa na upepo?" Si Yohana. La, la. Si Yohana, hamkuwa mnamsukuma kutoka mahali pamoja hadi pengine. Kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini, mtu mwenye ukosi uliopinduliwa, mwajua, na nguo nzuri na kadhalika?" Kasema, "Wanawabusu watoto wachanga, na kuoza, kuwazika wafu, nao ni wa ikulu za wafalme."

35 Hiyo ni...Hawajui, wao—wanachezacheza na kisu kidogo cha kukunja, hawajui jinsi ya kuchukua upanga ukatao kuwili, kusimama huko nje kwenye uwanja wa vita ambako unapigana na pepo, na kadhalika, huyo si mtu wa namna hiyo. Kasema, "Hamninii...Hilo silo mliloenda..." Kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini? Nabii?" Akasema, "Nawaambia, mkuu kuliko nabii." Alikuwa, alikuwa ni mjumbe wa agano, naye alikuwa mkuu kuliko nabii, aliwaunganisha hao pamoja.

36 Sasa, tunamwona Bwana wetu basi, katika kazi Yake kwamba alidai hatendi neno Mwenyewe ila lile alilomwona Baba akilitenda. Alimpa Mungu sifa zote, jambo ambalo halikuwa la kawaida, la kimbinguni.

37 Kila silaha tuliyo nayo, ndugu, silaha zetu zote ni za kimbinguni. Sisi—sisi...Hakuna kitu cha kawaida tulicho nacho. Ninii...Hatuna budi kuliamini. Tunda la Roho ni nini?

Upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, subira. Sasa, hebu shuka uende kwenye duka la dawa ukaninunulie subira yenye thamani ya robo, ninaihitaji, upendo wenye thamani ya dola tano, ningeweza kuvumilia mwingi wa huo. Unaona? Mnaona, ni kitu *fulani* kisichoonekana, hicho ndicho silaha zetu zote, tunasimama katika ulimwengu usioonekana tukiangalia mambo yasiyoonekana, hata hivyo, kwetu sisi, tunayaona, kwa sababu imani yetu inayatambua na kusema yapo, mnaona.

38 Na wakati Yesu. . .Siku moja ugonjwa ulikuja katika familia ya rafiki Yake, Naye akaondoka. Baba alikuwa amemwambia aondoke, maana Yeye alisema, Yohana Mtakatifu 5:19, Hakufanya neno mpaka Baba alipomwonyesha, si Baba *alipomwambia*, bali *alipomwonyesha*. Basi akaondoka.

39 Ndipo wale dada wazuri wa Lazaro wakatuma mtu Kwake na kusema, "Njoo umwombee rafiki Yako, yeye ni mgonjwa." Na badala ya kwenda kwa rafiki huyo mpendwa, na kuwasaidia wakati wa haja, baada ya wao kutoka makanisani mwao na kila kitu wapate kuwa wanafunzi Wake, Yeye alipuuza huo wito na kuendelea. Ndipo walipoagizia aitwe tena, badala ya Yeye kuitikia wito huo Yeye alienda mbali zaidi.

40 Sasa, ilionekana kana kwamba hilo linge—lingemrarua mtu yeyote. Mnaona? Lakini imani inaposhika kitu fulani, hakuna—hakuna cha kuizuia, itadumu papo hapo. Mnaona?

Sasa, aliporudi, hatimaye alisema, "Lazaro. . .amelala usingizi." Hivyo ndivyo alivyojua.

Lakini wanafunzi wakasema, "Kama, loo, kama amelala, anapumzika, anafanya vema."

Lakini ilimbidi kuwaambia katika lugha yao, "Amekufa. Na kwa ajili yenu nina furaha sikuwapo, lakini ninaenda kumwamsha."

41 Lakini Martha alipoona hilo, ya kwamba alikuwa ameingia mjini, alimwendea akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Mnaona?

Naye akasema, "Ndugu yako atafufuka tena."

42 Sasa, mkiangalia, wakati alipoenda kwenye kaburi ambapo Lazaro alikuwa. . .Sasa, Yeye tayari alikuwa. . .Alijua yale hasa yatakayotukia, nina hakika sote tunaamini hilo, alijua, maana Yeye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha, na hiyo ndiyo sababu hakwenda, hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Ni—nina furaha sikuwapo kwa ajili yenu," kwa sababu wangekuwa wakimsihi amwombee, wakati tayari Yeye alijua kwa ono kwamba hakupaswa kumwombea, alikuwa amfufue katika wafu. Mnaona? Naye akasema, "Ninaenda kumwamsha."

43 Lakini mnakumbuka, aliposimama kaburini alisema, "Wewe tayari . . . lakini kwa ajili ya *hawa* nilisema jambo hili," mnaona, kwa kuwa, mnaona, hilo, kwa mfano.

44 Ndipo akamwita Lazaro kutoka kaburini, mtu aliyekuwa amekufa siku nne, alimwita akarudi kuwa hai tena, naye akasimama kwa miguu yake akaishi. Hakuna hata jambo moja lililosemwa hapo kuhusu Yeye kudhoofika, ama kupata matokeo yoyote ya kimwili kutokana na jambo hilo. Kwa nini? Ilikuwa ni Baba akitumia Karama Yake Mwenyewe. Mungu alikuwa ndiyo kwanza amemwambia moja kwa moja.

45 Lakini akipitia kwenye umati wa watu siku moja, ambapo maskini mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi Lake, maskini mwanamke mmoja katika wakati wa kukoma hedhi alikuwa na mafuriko ya damu, na kwa hiyo akagusa vazi Lake, Naye akasimama na kusema, "Ni nani aliyenigusa? Naona kwamba nimekuwa dhaifu." Mnaona, hiyo ilikuwa ni yule mwanamke akitumia Karama ya Mungu. Mnaona? Yeye alikuwa ni Zawadi ya Mungu. Zawadi kubwa kuliko zote iliyowahi kutolewa kwa ulimwengu ilikuwa ni wakati Mungu alipomtoa Mwanawe. Sote tunakubali hilo. Mnaona? Basi mnaona, Mungu alikuwa akitumia Karama Yake.

46 Ni hivi tu: Sisi sote . . . Kuna kanivali mjini. Nasi maskini watu wa kusini, mwajua, hatukuwa na pesa zozote, na kwa hiyo tu—tunataka kuona maonyesho haya, ni kwenye ua mkubwa wa mbao. Naye Ndugu Williams hapa, tuseme yeye ni mfupi na mwenye nguvu, imara; nami ni jamaa mkubwa mno, mrefu, mwembamba. Na kwa hiyo, labda, huenda ikawa angeweza kuwapelekea ndovu maji, yeye ana nguvu. Nisingeweza kufanya hivyo, juu sana kutoka ardhini, mnaona, nisingeweza kubeba maji aliyoyabeba, maana ameumbwa mfupi na mwenye nguvu. Sasa, yeye hawezi kujizuia kuwa hivyo, wala mimi siwezi kujizuia kuwa jinsi nilivyo.

47 Na hivyo ndivyo kila moja ya huduma zetu. Mnaona? Hatuwezi kujizuia kuwa kile tulicho, "Mungu ameweka Kanisani . . . " Mnaona? Mungu alifanya hivyo kwa neema kuu.

48 Vema, sasa, sote tunashangaa ni kitu gani kilicho ng'ambo ya pazia lile pale. Hivyo ndivyo tulivyo, sote tunafanya leo. Ni kitu gani? Kuna nini huko ng'ambo? Tunakuja . . . Kama yule mfalme wa Uingereza, wakati ilipoitwa Nchi-ya malaika, wakati Mtakatifu Nikolasi alipokuja kule, naye akambatiza mfalme wa Uingereza katika Jina la Bwana. Wakati alipoketi kando ya moto usiku huo na shomoro mdogo akaingia kutoka gizani, akaruka ndani, akaruka-ruka, akarudi nje tena, Mtakatifu Nikolasi akamwambia, kasema, "Hivi alitoka wapi, na alienda wapi?" Mnaona? Hilo lilimshika mfalme. Kwa hiyo akambatiza mfalme, akaanzisha Ukristo huko Uingereza.

49 Sasa, wazo la, "Alitoka wapi?" Mahali ambapo anajua akili yake haiwezi kupafahamu, ndipo basi anafunga macho yake na kurudi mahali hapo. Yeye ana akili hapa, anajua, naye anajua ametoka mahali fulani, tena anajua anaenda mahali fulani, bali hajui ni wapi. Sasa, hilo ndilo sote tunalojaribu kuchunguza. Sasa, kila mmoja wetu ni wajumbe wa Nchi hiyo.

50 Sasa, tumesimama hapa asubuhi ya leo, nasi tunaangalia kila mahali, hakuna mahali tunapoweza kuingia chini yake, lakini hatimaye ninaangalia, na kuna shimo la fundo hapa juu, juu kabisa. Ninasema, "Ndugu Wilson . . . "

"Kamwe sitafaulu, Ndugu Branham. Nimeumbwa karibu sana na udongo, kamwe si—siwezi kulifikia."

51 Lakini nimeumbwa, tofauti kidogo, ninaweza kulifikia kama nitaruka juu, juu sana, na kulishikilia tu kwa vidole vyangu, na kujinyanyua juu, na kuangalia. Tunashangaa kuna nini upande huo mwingine. Sasa, hiyo ni njia fidhuli ya kulielezea, bali na—natumaini mnalielewa. Huo ndio msimamo asubuhi ya leo, tunaposimama pamoja, mnaona, una jambo la kufanya, nina jambo la kufanya.

52 Langu, nilizaliwa kuona maono. Sasa, jukwaani, huyu hapa anakuja . . . mtu fulani anakuja mbele yangu. Sasa, inahitaji imani yao kufanya hivyo, ni imani yao wenyewe. Sasa, ni kama tu gia, kuingiza gia, kubadilisha . . . unapanda kilimani kwa gari kisha unabadilisha gia. Unaona? Siwezi kubadilisha gia hiyo, Yeye huibadilisha. Mnaona?

53 Halafu basi, labda saa kadhaa kabla sijaja mkutanoni ni—niko katika maombi na pekee yangu, ndipo basi ninaona hiyo Nuru ikija karibu nami, basi hakuna mtu anayezungumza nami, ninaingia tu ndani. Ingekuwa afadhali kama ningeingia tu humu jengoni, pasipo kuongea wala chochote kile, niingie moja kwa moja kwenye mstari wa maombi, ingekuwa bora zaidi. Lakini badala ya kufanya hivyo, na—nazungumza kwa muda kidogo. Mikutano ya namna hiyo haingeweza kudumu muda mrefu sana, maana inaondoa uhai moja kwa moja kutoka kwako.

54 Lakini sasa, huyu hapa mtu amesimama, tumesimama hapa pamoja sasa, tunataka kuangalia ng'ambo ya pazia la wakati. Sasa, ninaruka kwa nguvu sana, ninakimbia juu namna *hii* na kushika, na kujinyanyua juu, narudi chini.

"Uliona nini, Ndugu Branham?"

"Ndovu."

"Loo, kweli?"

"Naam."

"Uliona nini tena?"

"Huyo tu ndiye niliyekuwa na wakati wa kumwona."

55 “Whiu!” Mwenye nguvu, mnaona, kama tu, lilinichosha. Ilikuwa ni kitu gani? Huyo ni mtu anayesimama mbele yangu. Mnaona, ni—ni wao wakitoa kitu fulani kutoka kwako, unaona.

“Uliona nini?”

“Una uvimbe. Uliniacha.” Mnaona? Ni uchovu, nilichoka.

56 “Uliona nini tena, Ndugu Branham?” Sina budi kwenda tena. Vema. Huyo unapanda juu tena, na kujinyanyua na kujitahidi, mwajua. Na muda si muda wajua, unarudi chini, “Wewe ni Binti *Nanii*, kutoka *ninii*. . . ” Mnaona? Haya basi. Unafanya hivyo mwenyewe, huyo ni wewe, si kunitumia mimi, bali ukitumia karama ambayo Mungu alituma kwa ajili yako, unaona. Unaona? Lakini sehemu ya kimwili inaumiza.

57 Sasa, vipi kama kiongozi wa hiyo sarakasi akipitia hapo, bosi wa kitu hicho chote? Aseme, “Unaangalia nini, Ndugu Branham? Naam, ninakujua. Ninataka kukuonyesha kitu fulani.” Anichukue tu, aniinue juu mkononi mwake, ama kitu kama *hiki*, na kusema, “Unaona hema hili? Watu hawa hufanya *hivi*, na kwenda *hapa* chini, na kushukia *hapa* chini, na *hapa* juu, na chini *pale*.” Nimeketi tu pale nikiangalia. Mnaona? Ni sawa. Ndipo anaporuhusu. . .ananiweka chini, sijachoka. Mnaona? Huyo ni Mungu akitumia karama Yake Mwenyewe. Mnaona ninalomaanisha? Hivyo ndivyo ifanyavyo.

58 Sasa, watu hapa, baadhi ya watu hawa walio pamoja nami. . .Labda baadhi yenu ni wageni kwangu. Lile ono linalotokea *huko* nje, wakati Yeye anapolituma tu kwa mamlaka makuu, hakuna malalamiko juu yake, wakati mwingine chini ya upako, bila pumzi mwilini mwako, au kupumua kwa dakika hamsini au sitini. Mnaona? Naye anasema yale yatakayotukia kikamilifu kabisa, mahali yatakapotukia, jinsi yatakavyotukia na kila kitu, mandhari yote ya kitu hicho chote. Huku Mungu akiwa Hakimu wangu, ambaye ninasimama katika Biblia Yake hapa, hajashindwa kamwe wakati mmoja hata nukta moja, ya maelfu ya nyakati. Na. . . Lakini hakuna malalamiko juu ya hilo.

59 Lakini katika mkutano wakati maskini mtu mdogo atakuja, kama, hiyo ni wao wakitumia karama iyo hiyo, mnaona, ni mtu huyo anayeitumia. Sasa, mnalipata? Yesu hakuhisi uchovu alipomfufua Lazaro kutoka kaburini, kwa sababu Baba alikuwa amemwambia. Mnaona? Lakini sasa, inapofikia mwanamke kutumia Karama hiyo, nguvu zilikuwa zimemtoka. Mnapata ninalomaanisha? Hilo ndilo linalolisababisha.

Na, enyi marafiki, ninyi watu ndio mnaofanya hivyo. Mnaona? Si mimi, ninyi ndio mnaolifanya, imani yenu.

60 Sasa, kuna jambo moja tu ambalo ningetaka kusema sasa, tena, maana labda watakuwa wakituondoa hapa. Lakini. . . Sasa angalieni kile lisemacho, msiondoke upesi sana. Mnaona? Ninii. . .Nadhani Ndugu Borders anaweza kuwaelezea hilo ka—katika kuifungua hii mikutano. Mnaona? Msiondoke haraka

sana. Inaposema, “Huyu hapa mtu ambaye. . .yuko mbele hapa. . .ana u—uvimbe, ama kansa, ama. . .”

61 Hapa, hebu niwape mfano kidogo, tuseme, tutamchukua Ndugu Williams hapa, nami nafikiri itatoa. . .Je, tuna wakati kiasi hicho? Tutaninii. . .Sekunde moja tu, ninii tu. . .

62 Sasa, sijawahi kumwona hapo kabla, tuseme sijawahi kumwona. Niko katika Jiji la New York. Naye anaenda hapa nje leo kwa daktari, naye amevaa suti hii nzuri, nyepesi na tai. Naye anaenda kwa daktari, ndipo daktari anasema, “Kasisi, ninasikitika sana kukwambia, lakini unaugua TB, hakuna kitu kinachoweza kukusaidia sasa. Uko—uko katika kiwango ambacho imechelewa sana kuutibu, kwa hiyo i—i—ita—itakuua.”

63 Vema, anaanza kushangaa. Mtu fulani. . .Imani yake inashika, “Naamini nitamwomba Ndugu Branham aniombee.” Anasikia habari zake. Anakuja New York, mimi niko New York. Na sasa amevaa su—suti nyeusi pamoja na tai nyekundu, naye amevua miwani yake, naye anapanda jukwaani. Nimesimama pale, sijawahi kumwona maishani mwangu, wala hajawahi kuniona, nasema, “U hali gani, Bwana?” Ninafanya nini? Kuwasiliana na roho yake. Mnaona? Ili tu kuona ni hisia ya namna gani, wakati mwingine tunakutana na wadanganyifu, tunakutana na wakosoaji. Tulikuwa na mmoja mkutanoni jana usiku, karibu tu anirarue vipande-vipande, na kwa hiyo hiyo ndiyo sababu nisingeweza kuitisha mstari huo wa maombi. Na, vibaya sana!

Na kwa hiyo basi nasimama pale na kusema, “Hujambo?”

Anasema, “Sijambo?”

64 Ninaendeleza maongezi, baada ya kitambo kidogo ninaona kitu mbele yangu, nikasema, “Unaugua ninii. . .” Nitachukua upambanuzi mzuri, mrefu. Tuseme hakuna mtu mwingine jukwaani ila yeye, mnaona, kuwa pale usiku huo. Nasema, “Unaugua kifua kikuu.”

“Hiyo ni kweli.” Mnaona?

65 “Sasa, ulikuwa kwa daktari. Huyo daktari alikuwa na masharubu, na alivaa miwani, na kichwa chenye mvi, naye alikuchunguza na kusema. . .Nawe hutoki hapa, unatoka kwenye nchi ambamo mna mchanga mwingi na—na kadhalika. Wewe. . .Ni California.”

“Naam, hiyo ni kweli.”

“Wewe ni mhudumu wa Injili.”

66 Mnaona? Ninaangalia tu yale anayofanya. Na labda nimekuja kwenye mkutano uu huu (na kunifanya mtu mwingine sasa), “Na hivi majuzi ulikuwa umevaa suti nyeupe, suti ya rangi nyepesi na tai nyepesi, ulikuwa umeketi mezani ukimsikiliza mtu fulani akizungumza, ulikuwa umevaa miwani. Mama fulani aliketi karibu nawe, ki—kidogo alikuwa mnene, alivaa nguo ya

waridi." Mnajua ilikuwa ni kweli wakati huu *hapa*. Mnaona? Nalo linaniacha tu, sijui nilichosema. Mnaona? Nilikuwa nimesimama papa hapa nikiangalia hilo.

67 Vema, labda amesisimkwa sana basi, "Mungu asifiwe! Hiyo ni kweli. Ni—nilikuwa nikimsikiliza Ndugu Branham akizungumza." Mnaona, kama . . . "Hiyo ni kweli kabisa! Nami nilikuwa nimevaa suti hiyo. Haleluya!" Huyu hapa anaondoka jukwaani.

68 Sasa, hajangojea muda mrefu vya kutosha. Mnaona? Yeye ananinii tu . . . Huyo ni yeye anayefanya hivyo, hilo ni lile imani yake mwenyewe ililofanya. Sasa, ngoja uone yale Mungu anayosema juu yake. Unaona? Sasa, kama hakuna kitu kingine kinachotukia, ninasimama hapo kwa dakika moja wala hakuna kitu kinachotendeka, ninaendelea kuangalia, kama hakuna kinachotukia, ninaangalia nyuma, na kama bado hajatiwa uvuli, nitasema, "Nitakuombea, Bwana," kisha nimwache aende.

69 Lakini ukimsikia akijibu na kusema, "BWANA ASEMA HIVI!" Unaona? Sasa, imani yako ndiyo iliyovuta *hilo* kutoka kwa Mungu, lakini sasa, *hapa* ni Mungu akikujibu. Unaona? Sijui kitakachotukia bado, maana mimi . . . hiyo ilikuwa ni imani yake mwenyewe iliyofanya hivyo, ambayo haikusema alikuwa ameponywa. Mnaona? Hiyo ilikuwa imani yake tu ikimfanya Mungu kufanya hivyo. Ilitabiri. Na sasa, ngoja mpaka itakapotabiri. Unaona? Ndipo inarudi, nami ninamwona labda miaka kadhaa baadaye, mtu mkongwe. Mnaona? Nami nasema, "Bwana, BWANA ASEMA HIVI, umeponywa. Kwa jambo hili, kuongeza imani yako, kesho uko katika mji wa kigeni. Utakuwa ukitembea mtaani, na mtu fulani atakugusa mkono, utageuka, atakuwa ni kijana muuza magazeti, nawe utaangalia saa, na itakuwa imefika saa sita, kamili. Kwa jambo hili utajua." Unaona? Sasa, moja ni kile alichovuta kutoka kwa Mungu, kilichofuata ni kile alichopewa na Mungu. Alifanya cha kwanza, sasa ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Hilo—hilo ndilo linalofuata, mnaona.

70 Ndipo—ndipo kesho yake ataenda, naye atawaambia marafiki waliokuwa pamoja naye, baadhi yenu ndugu wahudumu, "Hilo si lilikuwa ni ajabu?" Mnaona? Sasa, kama ni imani yake tu imefanya jambo fulani, anajua imani yake imemgusa Mungu, lakini sasa, Mungu amemwambia nini? Hajangojea muda mrefu kutosha kujua, mnaona, alikimbia moja kwa moja akatoka jukwaani.

71 Sasa, atazunguka kesho yake akisema, "Mnajua nini?" Ndipo kitu fulani kitamgusa, kasema, "Nini?" *Bang*, *bang*: saa sita. Kasema, "Kitu gani?" Mnaona? Loo, basi hakuna kitu kinachoweza kumfanya atilie shaka. Yeye ni . . . Limetia nanga moja kwa moja hapo. Mnaona?

72 Hapa, ninii tu. . . Ndugu Evans hapa, anayeketi papa hapa. . . Sasa, tunatambua ya kwamba hatupaswi kutumia karama za Mungu kama ubao wa kuwasiliana na pepo, tunatambua hilo. Hatuwezi kucheza na karama za Mungu, Yeye asingempa mtu yeyote ambaye angefanya hivyo. Hiyo ni kweli. Mtu huyu alikuwa amekuja kunitembelea, yeye na mke wake na watoto wake. Na kuna mengi tu yangeweza kusemwa kuhusu mengi ya mambo haya, lakini haya hapa yaliyotukia, kwa hiyo ushuhuda mdogo. Alikuwa na ga—gari jipya, nguo zao zote na kadhalika ndani yake, akasimama kwenye Mkahawa wa Miller huko Louisville. Na huko Kentucky, unaweza kuuza gari mradi tu una ninii. . . wewe. . . Watakutengenezea hatimiliki yake. Mnaona? Nao walikuwa na genge la wezi kule waliokuwa wakiiba magari, wakiyaleta na kuyapaka rangi tena, wakiyatengenezea hatimiliki, na kuyauza. Loo, walininii tu. . . lilikuwa ni jambo baya sana.

73 Bw. Evans, akija kwa mamia ya maili, yapata maili mia saba na hamsini kutoka Georgia, huko juu, aliingia tu akiendesha gari, akazima ufunguo, akaingia kula. Akarudi nje, gari, nguo, kinasasauti, kila kitu alichokuwa nacho kilikuwa kimevurugika, kimetoweka, hakujua lilikuwa wapi. Kwa hiyo huyo hapo, mamia ya maili kutoka nyumbani, hana pesa, hana nguo, hana chochote, na gari jipya limetoweka.

74 Vema, wakaambatana na Ndugu Sothmann, na ninaamini Ndugu Simpson, na baadhi ya ndugu pale. Kwa hiyo hatimaye wakasema, "Na tumtake Bwana shauri." Kwa hiyo wakasema, "Hebu tupande twende tukamwulize Ndugu Branham." Kwa hiyo wakaja nyumbani.

75 Na hayo ndiyo mahojiano ya faraghani yafanyayo, mnaona, tunakaa mbele za Bwana mpaka jambo fulani litukie. Sio kama kukutana nao jukwaani, ni wakati unapokaa pale na kungojea tu. Watu wanaketi pale kutoka ng'ambo na kote ulimwenguni, wakingojea, miadi mia tatu hivi ikingoja sasa, mnaona, kutoka kila mahali kutafuta kujua kuhusu mambo haya.

76 Na kwa hiyo, ndipo Ndugu Evans, na Ndugu Fred, na wengi wao wakaja nyumbani kule, ndugu wanne ama watano. Ndugu Willie, sijui kama ulikuwa pamoja nao asubuhi hiyo au la, ninajua Ndugu Fred alikuwako, nami siwezi kukumbuka walikuwa wangapi, ndipo tukainama mbele za Bwana kuomba.

77 Sasa, hawa wote ni wahudumu, ninatumaini, ninyi nyote ni waaminio. Mnaona, huna budi kutafuta kujua hali ya mambo, huna budi kutafuta kujua kiini chake kabla hujapata tiba, daima. Unaona? Daktari, ukienda ofisini mwake naye akasema. . . "Daktari, ninaugua, mimi. . . tumboni mwangu, ninaumwa na kichwa," akupe aspirini, akuache utoke, anajaribu kukuondosha. Unaona? Daktari halisi atauchunguza ugonjwa huo mpaka atakapopata kiini chake. Na hivyo ndivyo ilivyo

kupitia kwenye mstari wa maombi, kuwawekea watu mikono, ukisema, "Utukufu kwa Mungu. Haleluya! Liaminini. Utukufu kwa Mungu. Nitikise ninii yangu..." Mnaona? Hebu tupate kiini chake kwanza.

78 Huenda ikawa ni kitu fulani, Mungu aliweka laana juu ya mtu huyo kuwafanya wafanye jambo *fulani*, nawe unakuja, unaliondoa, kama vile Musa alivyoupiga ule mwamba, ama Eliya, ati kwa sababu aliitwa mwenye upara, akawalaani hao watoto wadogo, na kadhalika. Inakubidi kuwa mwangalifu kwa karama za Mungu, inakubidi kuangalia kile unachofanya, unaona, unapoanza kulaani na kuwakanyaga pepo, na mambo kama hayo, wakati hujui unachozungumzia, utapata shida na Mungu, unaona, maana inakubidi kutambua kilichotukia. Hiki...Kitu fulani kiko kule chini kikisababisha hili kutukia, basi afadhali ungojee na umwambie mtu huyo kulihusu, ulisahihishe hilo kwanza.

79 Kwa hiyo jambo la kufanya ni kungojea mpaka utakapopata kiini chake. Ndipo wewe...Tiba tayari ni kamilifu, kama u—unaweza kupata kiini chake. Ondoa kiini ndipo ninii...Kama vile, kama bonge limelalia kitu *fulani*, kama ki—kipande cha mahindi, na kijiti kimeyalalia, kikiyafanya yakue kombo, ondoa tu hicho kijiti nayo yatanyoka. Hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona? Huna budi kutafuta kujua kiini chake kwanza. Lakini tafuta kujua kinachoyafanya yafanye hivi.

80 Sasa, ndipo Bw. Evans akaingia, naye akasema, "Ndugu Branham," akasema. Akanisimulia hadithi hiyo.

81 Nikasema, "Hebu tumwendee Mungu." Ndipo tukapiga magoti kuomba. Na wakati tukiwa katika maombi mimi... Huna budi *kutoka nje*. Hiyo ndiyo njia ya kuwafufua wafu... Mmesikia juu ya mikutano, mmeiona, mnajua imeandikwa, taarifa za madaktari zilizotiwa sahihi za watu waliokufa. Nimewaona watano wa hao katika huduma yangu nyenyekevu. Huna budi kuipata nafsi hiyo iliyo huko nje mahali fulani, na kuirudisha, kuirudisha. Na kuhusu Roho *kutoka nje*, Yeye alilituma Neno Lake, alilituma Neno Lake. Mnaona?

82 Ndipo *nilipotoka nje*, nilimwona jamaa mdogo amevaa shati la manjano, wakati mmoja alikuwa Mkristo na kulelewa katika nyumba ya Kikristo, alikuwa kwenye gari la Ndugu Evans akishuka kwenda Bowling Green, Kentucky, maili mia moja na kumi na nane chini ya Louisville. Naye Roho, wakati nikiomba, alimsadikisha kwamba alikuwa akifanya makosa. Alikuwa akilifanyia kazi genge hili, alikuwa akifanya makosa. Ndipo Roho, Neno, likishikiliwa juu yake katika maombi haya, akageuka, akarudi.

83 Nilimwona akilirudisha hilo gari na kuliegesha mahali *fulani*. Nikasimama na kumwambia Ndugu Evans kuhusu jambo hilo, itakuwa sawa. Naye akienda zake nyumbani huko

kutoka . . . Sasa, gari liliibwa ng'ambo ya mto, Louisville, Kentucky, maili moja kuvuka mto, kisha huko juu kwenye Mkahawa wa Miller, liliibiwa kutoka huko. Na hapa likarudishwa kutoka Bowling Green, alikuwa na tangi zima la petroli, nusu yake imekwisha, mahali ambapo mvulana huyo alikuwa ameliendesha, akalirudisha tena, na kuliegesha papo hapo barabarani ambapo yeye . . . akienda zake moja kwa moja kwenye kambi ya trela kule akakutana nalo, limeegeshwa pale pale barabarani vivyo hivyo. Mnaona? Sasa, huyo ni Roho wa Mungu *akitoka nje* kulishika hilo.

84 Kisa kingine papo hapo, kuwaonyesha tu kinyume chake, kisha nitaondoka, hakika kabisa. Kwa hiyo basi wao . . . Huyu ni mtu yule yule, juu ya mtu aliyenunua gari kutoka kwake na wala asingeninii . . . hakumlipa, akatoroka. Naye Roho wa Bwana, tulipoomba, alimfuata mtu huyo, bali alikuwa ni mwenye dhambi mkali, mwovu. Mnaona? Neno lisingekuwa na athari kwake, basi ilimbidi Mungu kufanya kazi kwa njia nyingine, na kumtuma kote.

85 Basi siku moja alipokuwa huko nyumbani kwangu, nilimwambia, "Tunapitia Bowling Green." Tukishuka kwenda nyumbani kwake, tulikuwa tukishuka kwenda kuvua samaki, mimi na yeye na mke wake tukiwa kwenye gari, akalishika upesi sana.

Sasa, mimi . . . akasema, "Je, mimi . . . ? Afadhali nilisimamishe *hapa* chini."

Nikasema, "Kama unataka pesa zako, afadhali uende sasa." Naye akaenda kule, akalipwa zote. Mnaona?

86 Mnaona, Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo ili kulitatua. Mnaona? Lakini wakati mwingine kama ni kisa kinachoendelea . . . Sasa, kisa hicho kilidumu kwa miezi kadhaa au zaidi, miezi miwili . . . [Ndugu Evans anasema, "Miaka miwili."—Mh.] Ati wasemaje? ["Miaka miwili."] Miaka miwili kabla halijatendeka. Lakini mnaona, alikuwa ameuliza, na alijua ya kwamba kama tukiombea jambo hilo . . .

87 Martha alisema, "Ndugu yangu amekufa, ananuka huko nje kaburini. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Haya basi. Unaona? Unaona? "Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Miaka miwili baada ya yote aliyoshikilia, alijua angezipata. Mnaona? Mungu alilishughulikia moja kwa moja, akazipata.

Jambo ndilo hilo, ndugu, ni Mungu akijiakisi Mwenyewe maishani mwetu.

88 Ningeweza kuzungumza nanyi siku nzima, ninyi ni kundi zuri sana la watu, ninawapenda sana. Nami nipo hapa, marafiki zangu Wakristo, kuwasaidia. Nipo hapa kufanya yote niwezayo kuvuta juya pamoja nanyi ndugu.

89 Sasa, wakati mwingine watu husema sisi, hakuna mtu siku hizi, kumekuwako na uigaji mwingi wa kimwili wa mambo haya, mnaelewa hilo, hauna budi kuja tu. Musa alipojitokeza, mambo ya kimbinguni yalikuwa yamefanywa, na umati uliochanganyika ulienda pamoja naye, uliivuruga kambi baada ya kitambo kidogo na pamoja na Kora, mwajua, na kadhalika. Na sisi—sisi—sisi tunatambua jambo hilo, na linafanya hivyo, ndugu.

90 Nami. . . Wakati mwingine wachungaji hushuku kidogo, na mimi—mimi siwalaumu, wanao kondoo wa kuwalisha, mnaona. Wao—wao. . . Si—sina hisia yoyote dhidi ya ndugu hao ambao, hata wanaolihukumu, si—sijisikii vibaya juu yake, kwa sababu wao ni wachungaji, mnaona. Lakini nawatakeni mjue, kama ndugu yangu, wa—wakati mwisho ukikaribia, nitakapokutana nanyi Ng'ambo ya pili, ningali nitakuwa na ushuhuda ule ule: Ni Mungu. Wewe amini tu hilo kwa moyo wako wote.

91 Nami na—nawatakeni mniombee, ni vigumu sana, ndugu. Ni vigumu, maana wakati mwingine unasema. . . inakubidi kusema mambo ambayo. . . labda maoni ya mtu yamekuwa kwa njia moja, na hata hivyo huna budi kulisema, una—unawajibika kulisema, huna budi kulisema, halafu inaudhi, na inamwudhi labda ndugu yako ama kitu fulani, ndipo unajisikia vibaya sana juu yake.

92 Lakini wewe si mali yako mwenyewe, umenunuliwa kwa gharama, umeagizwa kwa kazi fulani. Inakubidi kuwa mwaminifu na mkweli kwake, haijalishi ni nini. Nami nafikiri karibu watu wote wenye akili timamu wataheshimu hilo, hata ingawa huenda wasikubaliane nawe, wataliheshimu.

93 Vipi kuhusu mwanamume kwa mwanamke? Haijalishi kama yeye ni mrembo, mwenye sura mbaya, ama chochote kile, kama yeye ni mama, mama halisi, mwanamume yeyote atamheshimu, aliye na wakia moja wa mwanamume ndani yake, mnaona. Haijalishi ni nani, anaheshimu msimamo wake. Mnaona? Na hivyo ndivyo ninavyofikiri ilivyo miongoni mwa ndugu, ndugu wanaomwona mtu ambaye ameshawishika. Nina heshima ile ile kwa ndugu ambao huenda wasikubaliane nami. Ni—ningesema, bila shaka ninaheshimu ninii yake. . .

94 Hadithi kuu inakuja akilini mwangu sasa ya yule mshauri wa Kilutheri kule juu, mwajua, aliponiandikia barua, na kusema nilikuwa mpiga ramli hodari, mwajua, na kadhalika namna hiyo, na kusema mabaya sana, mnaona, kunihusu mimi, hata hivyo, nilimwandikia barua kumjibu.

95 Akasema, "Ulisema ulikuwa ukihubiri kwa miaka thelathini," kasema, "Nilikuwa nikihubiri kabla hujaanza kunyonya," akasema. Halafu basi, na kusema jambo fulani na kama tu. . . Lakini hata hivyo, nilimheshimu. Yeye aliniita tu "Branham," nikamjibu, nikasema, "Ndugu Mpendwa wa Thamani," mshauri wa Kilutheri. Hakuna mtu angaliweza

kuihubiri Injili miaka hamsini na hata hivyo asimheshimu Kristo, nisingewazia hivyo. Mnaona? Yeye ni—yeye ni—yeye ni mwanadamu, ha—hajaumbwa kwa vumbi la mbao, yeye ni mwanadamu. Nami nikamwandikia barua nzuri kumjibu.

96 Naye akasema, "Wazo lenyewe la wewe kusimama kule juu! Mimi," kasema, "niliendesha gari maili kumi na tano kwenye mvua kubwa sana ya theluji kumsikia mtu wa Mungu, nami nilipata nini, ila mpiga ramli hodari."

97 Nami nikasema, "Ninakusamehe hilo, Ndugu," na kwa hiyo basi, nikasema, "hukujua ulilosema." Nikasema, "Watu walimwona Yesu Kristo akifanya jambo lile lile katika siku Zake kama afanyavyo katika siku zangu, ni Yesu yeye yule anayefanya jambo hilo, nao walimwita Beelzebuli."

98 Nikasema, "Sasa, vipi kama nilikuwa sahihi? Naye Yesu alisema kunena neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe." Nikasema, "Miaka yako hamsini imekufaa nini?" Mnaona? Mnaona? Nikasema, "Lakini ninajua hukumaanisha hilo kutoka moyoni mwako. Si—sidhani kabisa ya kwamba mtu angeweza kuzungumza juu ya Yesu kwa miaka hamsini, na kuhubiri kwa ajili Yake, awe mshauri wa chuo, angeweza kuzungumza juu ya Yesu namna hiyo. Unaninii tu . . . umesisimkwa tu wala huelewi."

99 Baadaye aliniandikia barua, akasema, "Ninaomba msamaha kwa hilo, nami ninasikia unakuja Minneapolis tena," ilikuwa ni Dk. Hegre, naye akasema, "Ni—nitaninii . . . Ni—ningetaka uje chuoni, ningetaka kukuuliza maswali kadhaa." Je, nina wakati wa kulisimulia? [Ndugu mmoja anasema, "Hakika."—Mh.] Sawa. Kisha akasema . . . Na . . . Nami nikasema . . .

100 Naye Ndugu Jack Moore na baadhi yetu huko juu, ilikuwa kwenye mkutano wa Wafanyabiashara. Naye akasema . . . Nikatoka nje. Na bila shaka, elimu yangu ni haba sana, kama mjuavyo, wala sidai kuwa mhubiri, kwa hiyo ni—nikaketi karibu na Ndugu Jack, naye ni mwerevu sana, mwajua, nami nikawazia kama alisema maneno fulani ambayo sikujua alichokuwa akisema, ningemgusa mguuni, naye angeshika hatamu kutoka hapo, mnaona.

101 Kwa hiyo wakatupa chakula kizuri cha jioni; wao ni Wanorwe. Na kwa hiyo walikuwa na mlo mkubwa mno wa kienyeji, nao wakaketi katika umbo la msalaba, na kuniweka kichwani mwake *hapa*, maskini wasichana hao wa kupendeza waliiandaa meza. Ndipo Dk. Hegre akasimama baada ya . . . baada ya chakula cha jioni akasema, "Ndugu Branham, najua huna budi kurudi kwa ajili ya ibada usiku wa leo, lakini," kasema, "ninataka kukuuliza swali."

Nikasema, "Dk. Hegre," nikasema, "Ningeninii . . . nitafurahi kujibu yale niwezayo. Labda, elimu yangu ni haba sana, huenda ni—nisiweze."

Akasema, “Vema, ningetaka kukwambia hili,” akasema, “Naomba msamaha kwa yale niliyosema.”

Nikasema, “Loo, ulisamehewa, Ndugu, nisingewazia, hilo.”

102 Naye akasema, “Tuna njaa hapa Be—Bethany,” akasema, “tu—tunamtaka Mungu,” akasema, “nasi tulisoma kuhusu Wapentekoste.” Naye akasema, “Nilisikia ya kwamba ulikuwa Mbaptisti.”

Nikasema, “Naam.”

103 Naye akasema, “Vema,” akasema, “nilienda kuwaona,” kisha kasema, “kulikuwa na mkutano,” kasema, “walikuwa wakipiga teke viti, na kuvunja taa za dirishani, na—na kadhalika namna hiyo.” Kasema, “Wana nini?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.”

Naye akasema, “Roho Mtakatifu hufanya hivyo?”

104 Nikasema, “Ndugu, haya ndiyo ninayokuta miongoni mwa Wapentekoste: Ni mvuke mwingi sana nao wanaupulizia kwa filimbi, badala ya kuuweka katika utaratibu na ku—kuutendesha kazi, mnaona,” nikasema, “wao, laiti wangejua jinsi ya kuufanya utende kazi! Wanautoa wote kwa makelele,” mnaona, “wanautoa kwa kupiga mayowe.”

105 Mnajua ninalomaanisha, na hiyo ni kweli. Sisemi hilo kwa kuwakosea heshima, ninalisema kwa upendo na heshima. Nguvu zilizoko Kanisani, laiti zingewekwa tu kazini, na kuwekwa kazini, kama umeme wa zigizaga unaoandika wa—wa—wakati wa mwisho kote angani, uingizeni kazini huo mwone utakalofanya. Mnaona? Edison alisema angeweza kufanya hivyo, naye akafanya hivyo. Mnaona? Ni, kuzifanyisha kazi nguvu hizi tulizo nazo. Mnaona, tunazipigia makelele tu, na kuzilipua. Mnaona?

Naye akasema, “Basi sisi Walutheri tuna nini?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu,” ndipo akachanganyikiwa kabisa. Nilifikiri . . . nikasema . . .

106 Akasema, “Nilienda California, nikaandika ninii . . . nilisoma kitabu wakati mmoja juu ya karama zote za kiroho.” Kasema, “Tuna njaa hapa Bethany,” naye akasema, “wenzangu wote hapa,” basi kulikuwako na yapata mia tatu ama mia nne wa hao wameketi pale, akasema, “sote tuna njaa kwa ajili ya Mungu.”

107 Akasema, “Sasa, jambo ni kwamba,” akasema, “tuliandika . . . tulisoma kitabu hiki shuleni mwetu, katika masomo yetu hapa.” Kisha kasema, “Mimi na baadhi ya ndugu tukapanda ndege, tukaenda California tukakutana na mtu huyu, naye akasema, ‘Sina karama zozote, niliandika tu habari zake.’”

108 Kasema, “Ndipo tukasikia kwamba ulikuwa ukija huku,” kisha kasema, “tukaenda kule.” Kisha kasema, “Upesi, tukiwa tumevunjika moyo mara nyingi sana kwa udanganyifu, tukalihesabu kwamba ni pepo mchafu ambaye. . .Nasikitika kwamba nililisema hilo.”

109 Nikasema, “Vema, hilo ni sawa.” Nikasema, “Sisi sote, labda, tuna nyakati hizo, Bwana.” Nikasema, “Labda imekuwa, huenda nilifanya jambo lile lile mimi mwenyewe, wakati mmoja.” Nikasema, “Mungu anaturehemu, bila shaka Yeye ananirehemu.”

Naye akasema, “Vema, ningetaka tu kusema jambo moja.” Akasema, “Tufanye nini?”

110 Ndipo ilitokea niliwazia, wale wanafunzi ambao hawangeweza kulipia masomo yao, walikuwa na shamba la kama ekari elfu moja kule, ama zaidi, labda ekari elfu mbili, nao wakapanda mahindi, na kuwaacha wanafunzi walifanyie kazi. Mnaona? Nami nikasema, “Wakati mmoja kulikuwa na mtu aliyepanda shamba la mahindi.” Ni wangapi wamewahi kuona mahindi yakichipuka? Sote tumeona. Nami nikasema, “Kesho yake asubuhi alipotoka kwenda kule kulikuwako na majani mawili madogo, ama, asubuhi moja wakati alipotoka kwenda kule kulikuwa na majani mawili madogo yametokeza. Akasema, ‘Bwana asifiwe kwa ajili ya zao la mahindi!’”

Nikasema, “Alikuwa nalo?”

Akasema, “Vema, nisingesema alikuwa nalo.”

Nikasema, “Hebu tuseme hivi: kwa uwezekano alikuwa nalo.”

“Naam,” akasema.

111 Nikasema, “Hao walikuwa ni Walutheri. Hatimaye, majani hayo mawili madogo yakakua yakawa kishada, kitu tofauti, basi hao walikuwa Wamethodisti kwa utakaso, ambapo ninyi nyote mlihubiri kuhesabiwa haki. Ndipo kishada kikainama tena kuliangalia jani na kusema, ‘Huh! Mimi ni kishada, sina haja na wewe hata kidogo, mimi *ndimi* sasa.’”

112 “Lakini mnajua, kishada hicho hatimaye kilipukutisha vishada hivi vidogo chini kwenye hilo jani tena, nacho kikazaa suke la mahindi, kama ile punje asili iliyopandwa.” Nikasema, “Hiyo ilikuwa ni Pentekoste, kule kurudishwa kwa karama zikirudishwa Kanisani.” Nikasema, “Tuna kuvu nyingi sana kwenye suke, lakini hata hivyo, tuna Punje humo pia, mnaona.” Nikasema, “Hiyo—hiyo ni kweli.” Nikasema, “Ilikuwa ni—ilikuwa ni. . .Pentekoste asili.”

113 Ndipo nikasema, “Ndipo ile Punje ikasema, ‘Sihitaji kishada wala jani. Siwahitaji ninyi Wamethodisti, wala ninyi Walutheri yeyote wenu, mimi ndiye Punje.’” Nikasema, “Hata hivyo, ilihitaji uhai uliokuwa kwenye jani kufanya kishada, na

uhai kwenye hilo jani kufanya punje." Nikasema, "Kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoboreshwa."

114 Akairudisha sahani yake upesi. Nikafanya jambo dogo rahisi namna hiyo, sio kubishania theolojia yao, mnaona, wala kubishana nao, kuwaacha tu waone ukweli ni upi. Mnaona? Hebu ninii. . . Akasema, "Ndugu Branham, sisi wa Bethany, haidhuru Walutheri wengine wanasema nini, tunamtaka Mungu. Tufanye nini tupate kumpokea Roho Mtakatifu?"

115 Nikasema, "Rudini nyuma kutoka mezani, igeuzeni migongo yenu ielekee mezani na kupiga magoti huku nyuso zenu zikielekea ukutani." Nasi tukazunguka na kuwawekea mikono, ndipo mia nne wakampokea Roho Mtakatifu, na sasa wamefikia mamia na mamia, wakifanya miujiza, na ishara, na maajabu. Huyo ni Dk. Hegre wa Chuo cha Bethany huko Minneapolis, Minnesota.

116 Ndugu, tuna bidhaa iliyo bora kuliko zote ulimwenguni, lakini tunaitumia vibaya, mnaona. Hiyo ni kweli. Mwasemaje, kama—kama Ndugu Borders hapa ni seremala, vipi kama alikuwa amesimama hapa nje na nyundo, akipigilia misumari kila mahali, mnaona, nami nilikuwa na na—namna fulani ya nyundo kubwa sana hapa, ambayo ningeweza kuweka pipa la misumari ndani yake, na kuipigilia *rruuut*, nipande tu namna hiyo, na kuzipigilia mbao zote mara moja, nami nimjie, niseme, "Naam, huko kwenye mashindano, huna chochote. Huna faida kwa vyovyote vile, ninii tu, hata huko kwenye mashindano"? Mnaona? Nimeharibu bidhaa yangu papo hapo, nimemwendea kwa njia mbaya. Mnaona?

117 Kama nikipanda na kumwambia alivyo seremala mzuri sana wa ajabu na kuiacha tu bidhaa yangu, itajiuza kama inafaa kitu. Hiyo ni kweli, mnaona. Na hilo ndilo lililonileta hapa, ewe rafiki, unaona. Ni kuninii. . . Bidhaa ya Mungu ambayo imeboreshwa, tungeiita, labda, huduma kwa Mlutheri, nanyi Wamethodisti, na Wabaptisti, na wengi wenu ndugu. Hatujaribu kuwasukumia kitu fulani, tunajaribu tu kuwaambia juu ya Karama iliyoboreshwa ambayo Bwana amelipa Kanisa, basi neema Yake na itusaidie.

118 Samahani, kuchukua wakati huu wote, nikianza tu kuzungumza. Mungu awabariki. Hebu tuimbe kwa urahisi sana wakati tukifunga mlango huu hapa sasa, tukifunga mlango.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

119 Sasa, huku tukiweka msingi huu mdogo wa uponyaji. . . Sasa, usiku wa leo, kama ni sawa kwa wachungaji na wote, ninataka kuchukua usiku mmoja kwa ajili ya wokovu, mnaona.

Kuninii...Mnaona, mnaona, hata hivyo, watu hawa ambao wameponywa, wataninii, kama wakiishi muda mrefu vya kutosha labda watakuwa wagonjwa tena, lakini kama wakati mmoja wakiokoka, wanao Uzima wa Milele basi, hiyo ni kweli, watakuja katika ule ufufuo.

120 Sasa, Yesu...Tumefunga milango na kumwomba Baba yetu, Yule aonaye kwa siri. Tunaweza tu kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo sasa, kwa ajili ya maombi?

121 Baba wa Mbinguni, kwa wasiwasi, kwa haraka, hatuwezi kuitendea hii kazi haki, bali natumaini ya kwamba kwa namna fulani, asubuhi ya leo, kwa Uwepo Wako kuwa hapa, kwamba sisi, tukiondoka hapa, tutaenda tu huku mioyo yetu imejaa furaha.

122 Wabariki watu hawa wema, Bwana, waliotukubalia kupata mahali hapa kwa ajili ya mkutano huu. Tunaomba ya kwamba watafanya kazi kubwa. Wanaonekana kwamba walikuwa wazuri, sisi, kundi la watu waliokataliwa, waliodharauliwa na ulimwengu, na hata hivyo walifungua milango na kuturuhusu kuingia, tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, wabariki. Na jalia kila mmoja...Jalia mtu huyu anayemiliki mahali hapa, msaada wote, jalia kuwe na ushawishi mkubwa wakati hao wahudumu wa kike wanapoingia kwenye chumba hiki, kwamba machozi ya huzuni kwa ajili ya dhambi yatatiririka mashavuni mwao. Jalia, Bwana, kwamba wote wataokolewa na kujazwa na Roho, wawe nguvu kuu kwa ajili ya Mungu.

123 Asante kwa ajili ya udugu huu, wanaume na wanawake hawa wazuri, ambao ninatarajia kuishi nao katika Umilele, katika nyakati zote zijazo, ama ulimwengu usio na mwisho. Mbariki ndugu yetu mwenyekiti hapa na mkewe, kila mhudumu na mkewe, wageni wote pamoja nasi asubuhi ya leo.

124 Na, Baba, katika wakati huu mkuu tunaoishi, kwenye wakati tu wa kushuka kwa nuru za jioni, jua linatua hapa kwenye Pwani ya Magharibi, hivi karibuni kutakuwa na siku ya taabu ambayo haijawahi kujulikana kamwe, ndipo "aliye mchafu, angali mchafu; aliye mtakatifu, angali mtakatifu." Mungu tujalie ya kwamba tutafanya kila kitu kilicho ndani ya uwezo wetu kumwingiza kila mtu katika Ufalme wa Mungu kabla haijachelewa sana. Mungu tujalie.

125 Bariki huduma ya hawa ndugu zangu, Mungu, maskini makanisa yao, na dada zangu na ndugu zangu wanaoketi hapa asubuhi ya leo, kazi zao. Mungu, wako hapa. Nimekutana na kundi hili dogo la Kipentekoste ulimwenguni kote, huko nyuma kabisa kwenye misitu hiyo kule, ambako watu wangethubutu kwenda, na kungekuwako na Mpentekoste mdogo asiyedhaminiwa ameketi kule nyuma akishikilia mshumaa wa Nuru, hashughulikiwi na mtu yeyote, maskini mwanamume ama mwanamke aliyesimama kule nyuma

ameharibika sura kabisa, naye ameliwa na ameba, huku nguo zimechakaa, lakini akishikilia mshumaa wa Nuru. Kama Paulo alivyosema katika Waebrania, "Watu ambao ulimwengu haustahili kuwa nao, walizunguka-zunguka wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi na wakiwa wahitaji na walioteseka." Mungu, ile—ile Hukumu kuu italifunua tu.

126 Jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya wanaume na wanawake kama hao, na kwa kushirikishwa na kundi kama hilo, kuketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu! Wabariki wote, Baba. Tunaomba ya kwamba neema Yako na rehema zitakaa juu yao.

127 Tusamehe udhaifu wetu mwingi, Bwana. Hatukusudii kufanya lolote baya, Bwana, bali kupitia mwili tunafanya makosa kila siku, kwa hiyo ili tudumu hai katika Kristo, inatubidi kufa kwa mawazo yetu wenyewe, hivyo basi tudumishe tumekufa kwa nafsi zetu na hai katika Yeye. Jalia miili yetu iwe hivyo, na nafsi yetu itiishwe Kwake sana hata watu wataona uakisi wa Kristo tunapoenda, ama tunapokuja, ama chochote tufanyacho.

128 Tubariki pamoja, Baba. Tusaidie usiku wa leo katika ibada, tusaidie kesho, saidia shule za Jumapili, makanisa. Na jalia kuwe na Moto wa Mungu katika kila kanisa na kila moyo mpaka Yesu atakapokuja. Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Tunairudisha kwa mwenyekiti, na, ndugu.

62-0630B Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo
Villa Motel
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org